06

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR

## JUNI, 2026

**24 JULAI, 2026**

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWEZI WA JUNI,2026

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa kuimarisha takwimu za jinsia nchini ikiwemo kukusanya, kuchambua na kutoa takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za udhalilishaji wa kijinsia hapa Zanzibar. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu 21.


## LENGO

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za udhalilishaji wa kijinsia ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

## MATUKIO YA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA YALIYORIPOTIWA POLISI JUNI 2026


Jumla ya matukio 143 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Juni, 2026 ambapo waathirika walikuwa 143. Waathirika wengi walikuwa watoto (waathirika 122 sawa na asilimia 85.3), wakifuatiwa na wanawake 17 (asilimia 11.9) na wanaume walikuwa wanne (4) sawa na asilimia 2.8. Miongoni mwa waathirika watoto 122, wasichana walikuwa 105 (asilimia 86.1) na wavulana walikuwa 17 sawa na asilimia 13.9 ya waathirika watoto wote.

**Kielelezo 1.1: Idadi ya Waathirika wa Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia, Juni 2026**




Idadi ya Matukio ya kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 78, ambapo waathirika 71 walikuwa wasichana na saba (7) wanawake. Matukio ya kulawiti/kunajisi yalikuwa 13 ambapo waathirika 11 walikuwa wavulana na wawili (2) wanaume. Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile yalikuwa 13 ambapo waathirika wote walikuwa wasichana. Matukio ya kutorosha yalikuwa tisa (9) ambapo waathirika wote walikuwa wasichana. Matukio ya lugha ya matusi yalikuwa tisa (9) ambapo waathirika watatu (3) walikuwa wanawake, waathrika wawili (2) wasichana na waathirika wanne (4) walikuwa wavulana. Matukio ya shambulio la aibu/kukashifu yalikuwa 15 ambapo waathirika wanne (4) walikuwa wanawake, waathirika tisa (9) walikuwa wasichana na waathirika wawili (2) walikuwa wavulana. Tukio la kutelekeza watoto lilikuwa moja (1) ambapo mwathirika ni msichana. Tukio la kuingilia maharimu lilikuwa moja (1) ambapo mwathirika alikuwa mwanamke, matukio ya mauaji yalikuwa mawili (2) ambapo waathirika wote walikuwa wanaume, na matukio ya kumpa na kupokea ujauzito yalikuwa mawili (2) ambapo waathirika wote walikuwa wanawake.

**Kielelezo 1.2 Idadi ya Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Aina ya Matukio Juni, 2026**



Wilaya ya Magharibi 'B' imeripotiwa kuwa na matukio mengi (matukio 26) sawa na asilimia 18.2 ikifuatia Wilaya ya Magharibi 'A' ambayo imeripotiwa matukio 24 (asilimia 16.8). Wilaya ya Kusini imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio(matukio (3)) sawa na asilimia 2.1 ya matukio yote yaliyoripotiwa.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Juni, 2026**



Idadi ya matukio ya udhalilishaji kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 11.7 kufikia matukio 143 kwa mwezi Juni, 2026 ikilinganishwa na matukio 128 yaliyoripotiwa mwezi wa Mei, 2026. Matukio yaliyoripotiwa kupungua kwa mwezi Juni, 2026 yalikuwa matukio ya kujaribu kubaka, kutupa watoto, kutorosha, lugha ya matusi na shambulio la mtoto. Wilaya ya Magharibi 'B' imeripotiwa kuwa na idadi kubwa(matukio 26) ya matukio kwa mwezi wa Juni, 2026 na Wilaya ya Magharibi 'A' ilikuwa na idadi kubwa ya matukio kwa mwezi wa Mei, 2026 (matukio 25).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mei 2026 na Juni, 2026**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kujaribu Kubaka | | Kutupa Watoto | | Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | |
| | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 |
| Kaskazini 'A' | 6 | 13 | 3 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 8 | 4 | 6 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 13 | 18 | 9 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kusini | 2 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Mjini | 20 | 23 | 10 | 12 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 2 | 2 | 0 | 2 |
| Magharibi 'A' | 25 | 24 | 7 | 9 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 3 | 3 | 5 | 3 |
| Magharibi 'B' | 24 | 26 | 10 | 13 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 4 | 4 | 6 | 2 | 0 |
| Wete | 12 | 8 | 7 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 |
| Micheweni | 4 | 4 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 6 | 12 | 3 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Mkoani | 8 | 8 | 7 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **128** | **143** | **65** | **78** | **1** | **0** | **1** | **0** | **9** | **13** | **10** | **13** | **11** | **9** |

**Inaendelea....Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mei 2026 na Juni, 2026**

| Wilaya | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Lugha ya Matusi | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Kutelekeza Watoto | | Mauaji | | Kuingilia Maharimu | | Kumpa na Kupokea Ujauzito | | Shambulio la Mtoto | |
| | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 4 | 3 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 3 | 3 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 3 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **13** | **9** | **15** | **15** | **1** | **1** | **0** | **2** | **0** | **1** | **1** | **2** | **1** | **0** |

Idadi ya matukio ya udhalilishaji kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 47.4 na kufikia matukio 143 kwa mwezi Juni, 2026 kutoka matukio 97 yaliyoripotiwa mwezi wa Juni, 2025. Matukio mengi yameripotiwa kuongezeka kwa mwezi Juni, 2026 isipokuwa matukio ya kutorosha, uzinifu na usumbufu wa kingono. Wilaya ya Magharibi 'B' imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio kwa Juni, 2026 (matukio 26) ikilinganishwa na mwezi wa Juni, 2025 ambapo wilaya ya Magharibi 'A' ilikuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 23).

**Jadweli 1.3: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Juni 2025 na Juni 2026**

| Wilaya | Idadi ya matukio | | Aina ya udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kujaribu kubaka | | Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Lugha ya Matusi | |
| | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 |
| Kaskazini 'A' | 2 | 13 | 2 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 8 | 4 | 7 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 6 | 18 | 3 | 10 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 14 | 23 | 8 | 12 | 0 | 0 | 3 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 3 |
| Magharibi 'A' | 23 | 24 | 10 | 9 | 0 | 0 | 2 | 2 | 2 | 3 | 1 | 3 | 0 | 3 |
| Magharibi 'B' | 18 | 26 | 10 | 13 | 0 | 0 | 1 | 4 | 2 | 6 | 1 | 0 | 0 | 3 |
| Wete | 7 | 8 | 5 | 5 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Micheweni | 9 | 4 | 7 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 7 | 12 | 2 | 8 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 4 | 1 | 0 | 0 |
| Mkoani | 2 | 8 | 1 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **97** | **143** | **56** | **78** | **0** | **0** | **7** | **13** | **5** | **13** | **10** | **9** | **0** | **9** |

**Inaendelea....Jadweli 1.3: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Juni 2025 na Juni 2026**

| Wilaya | Aina ya Matukio ya Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Kutelekeza watoto | | Mauaji | | Kuingilia maharimu | | Kumpa na kupokea ujauzito | | Uzinifu | | Usumbufu wa kingono | |
| | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 2 | 2 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 6 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **14** | **15** | **0** | **1** | 1 | **2** | **0** | **1** | **2** | **2** | **1** | **0** | **1** | **0** |

Miongoni mwa waathirika watoto 122 waliofanyiwa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Waliobakwa walikuwa wasichana 71, waliolawitiwa/kunajisi walikuwa wavulana 11, kuingilia kinyume na maumbile walikuwa wasichana 13, kutorosha walikuwa wasichana tisa (9), shambulio la aibu/kukashifu wasichana walikuwa tisa (9) na wavulana wawili (2), lugha ya matusi wasichana wawili (2) na wavulana wanne (4) na kutelekeza watoto alikuwa msichana mmoja (1).

**Jadweli 1.4: Idadi ya Matukio na Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya Juni, 2026**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti/Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Lugha ya matusi | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Kutelekeza Mtoto | | Kutupa Watoto | | Shambulio la mtoto | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 9 | 7 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 14 | 10 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 20 | 11 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 19 | 7 | 2 | 3 | 3 | 0 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 25 | 13 | 4 | 6 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 7 | 5 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 10 | 6 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 8 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **122** | **71** | **11** | **13** | **9** | **0** | **2** | **4** | **9** | **2** | **1** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |

Miongoni mwa wanawake 17 ambao ni waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; waliobakwa walikuwa saba (7), Kuingilia maharimu alikuwa mmoja (1), Lugha ya matusi watatu (3), Shambulio la aibu/Kukashifu walikuwa wanne (4) na Kumpa na kupokea ujauzito walikuwa wawili (2).

**Jadweli 1.5: Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Juni, 2026**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya udhalilishaji | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia maharimu | Kutorosha | Lugha ya matusi | Shambulio la aibu/Kukashifu | Kumpa na Kupokea ujauzito | Uzinifu |
| Kaskazini 'A' | 4 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 0 | 0 | | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Magharibi 'A' | 5 | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 |
| Magharibi 'B' | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **17** | **7** | **1** | **0** | **3** | **4** | **2** | **0** |

Kwa mwezi wa Juni 2026, idadi ya waathirika wanaume walikuwa ni wanne (4), waathirika wawili (2) wa tukio la kulawiti na waathirika wawili (2) wa tukio la mauaji.

**Jadweli 1.6: Aina ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Juni, 2026**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya udhalilishaji | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti/Kunajisi | Lugha ya matusi | Shambulio la aibu/Kukashifu | Mauaji | Kumpa na Kupokea ujauzito | Wizi wa watoto |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 3 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | | 0 |
| Wete | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **4** | **2** | **0** | **0** | **2** | **0** | **0** |

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 78) sawa na asilimia 63.9 ya matukio yote ya watoto yaliyoripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 32) sawa na asilimia 26.2. Matukio manne (4) sawa na asilimia 3.3 yaliripotiwa kwa umri wa miaka 6-10 na umri wa miaka 0-5, yaliripotiwa matukio nane (8) sawa na asilimia 6.6. Aidha idadi kubwa ya matukio ya kubaka yameripotiwa umri wa miaka 15-17 (matukio 54) sawa na asilimia 76.1 kati ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.7: Aina ya Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto na Umri Juni, 2026**

| Umri | 0-5 | | 6-10 | | 11-14 | | 15-17 | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** |
| Kubaka | 1 | | 1 | | 15 | | 54 | | 71 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 2 | | 1 | | 6 | | 2 | | 11 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 2 | | 2 | | 2 | | 7 | | 13 | |
| Kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 5 | 0 | 9 | 0 |
| Lugha ya matusi | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 4 | 2 | 4 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 0 | 2 | 0 | 0 | 4 | 0 | 5 | 0 | 9 | 2 |
| Kutelekeza mtoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kutupa Watoto | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la mtoto | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla ya Waathirika** | **4** | **4** | **3** | **1** | **26** | **6** | **72** | **6** | **105** | **17** |

Idadi ya matukio ya watoto waliopitia udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 11.9 kufikia matukio 122 kwa mwezi wa Juni 2026 ikilinganishwa na matukio 109 yaliyoripotiwa mwezi wa Mei 2026. Matukio mengi yameripotiwa kuongezeka kwa watoto mwezi Juni 2026 isipokuwa matukio ya kutupa watoto, kutorosha, lugha ya matusi na shambulio la mtoto.

**Jadweli 1.8: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri na Aina ya Matukio, Mwezi Mei, 2026 na Juni, 2026**

| Miaka | Kubaka | | Kutupa watoto | | Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Lugha ya matusi | | Kutelekeza watoto | | Shambulio la mtoto | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mei - 26 | Juni - 26 | Mei - 26 | Juni - 26 | Mei - 26 | Juni - 26 | Mei - 26 | Juni - 26 | Mei - 26 | Juni - 26 | Mei - 26 | Juni - 26 | Mei - 26 | Juni - 26 | Mei - 26 | Juni - 26 | Mei - 26 | Juni - 26 | Mei - 26 | Juni - 26 |
| 0-5 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 6 | 8 |
| 6-10 | 0 | 1 | 0 | 0 | 6 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 4 |
| 11-14 | 12 | 15 | 0 | 0 | 2 | 6 | 3 | 2 | 1 | 4 | 1 | 4 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 22 | 32 |
| 15-17 | 48 | 54 | 0 | 0 | 0 | 2 | 7 | 7 | 8 | 5 | 3 | 5 | 4 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 70 | 78 |
| **Jumla** | **60** | **71** | **1** | **0** | **9** | **11** | **10** | **13** | **10** | **9** | **10** | **11** | **7** | **6** | **1** | **1** | **1** | **0** | **109** | **122** |


Idadi ya matukio ya watoto kwa mwaka yameongezeka  kwa asilimia 47.0 na kufikia matukio 122 kwa mwezi wa Juni 2026 ikilinganishwa na  matukio 83 yaliyoripotiwa kwa mwezi wa Juni 2025. Matukio yaliyoripotiwa kupungua kwa mwezi Juni 2026 ikilinganishwa na Juni 2025  ni matukio ya kutupa watoto,kutorosha, lugha ya matusi na shambulio la mtoto.

**Jadweli 1.9: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri, Mwezi Juni, 2025 na Juni, 2026**

| Miaka | Kubaka | | Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Lugha ya matusi | | Kutelekeza watoto | | Usumbufu wa kingono | | Kutupa watoto | | Shambulio la mtoto | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Juni - 25 | Juni - 26 | Juni - 25 | Juni - 26 | Juni - 25 | Juni - 26 | Juni - 25 | Juni - 26 | Juni - 25 | Juni - 26 | Juni - 25 | Juni - 26 | Juni - 25 | Juni - 26 | Juni - 25 | Juni - 26 | Juni - 25 | Juni - 26 | Juni - 25 | Juni - 26 | Juni - 25 | Juni - 26 |
| 0-5 | 1 | 1 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 8 |
| 6-10 | 3 | 1 | 1 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 4 |
| 11-14 | 9 | 15 | 3 | 6 | 1 | 2 | 3 | 4 | 4 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 32 |
| 15-17 | 38 | 54 | 1 | 2 | 3 | 7 | 7 | 5 | 0 | 5 | 0 | 5 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 50 | 78 |
| **Jumla** | **51** | **71** | **6** | **11** | **5** | **13** | **10** | **9** | **10** | **11** | **0** | **6** | **0** | **1** | **1** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **83** | **122** |

Matukio mengi (matukio 78) yametokea nyumbani kwa mtuhumiwa sawa na asilimia 54.5 ikifuatiwa na idadi ya matukio yaliyotokea majumba mabovu (matukio 20) sawa na asilimia 14.0 na vichakani (matukio 17) sawa na asilimia 11.9 ikilinganishwa na maeneo mengine yaliyoripotiwa kwa mwezi Juni 2026.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea Juni, 2026**





Matukio 122 kati ya matukio 143 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 85.3 ya matukio yote yaliyoripotiwa, aidha matukio 13 yamepelekwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (asilimia 9.1), matukio manne (4) yamepewa hati ya mashtaka (asilimia 2.8), matukio mawili (2) yapo mahakamani (asilimia 1.4) na matukio mawili (2) yamefungwa na polisi (asilimia 1.4).

**Jadweli 1.10: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa Juni, 2026**

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | Waathirika | | Waathirika | | Hatua Zilizofikia | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Watoto | | Watu Wazima | | Zilizo Mahakamani | Zilizoti wa hatiani | Ziliachi wa huru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Offisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi | Hati ya Mashtaka |
| | | Wasichana | Wavulana | Wanawake | Wanaume | | | | | | | |
| Kubaka | 78 | 71 | | 7 | | 2 | 0 | 0 | 1 | 8 | 67 | 0 |
| Kulawiti/Kunajisi | 13 | | 11 | | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 10 | 1 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 13 | 13 | | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 9 | 0 |
| Kutorosha | 9 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 |
| Lugha ya matusi | 9 | 2 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 15 | 9 | 2 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 | 0 |
| Kutelekeza mtoto | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kuingilia maharimu | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Mauaji | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Jumla | **143** | **105** | **17** | **17** | **4** | **2** | **0** | **0** | **2** | **13** | **122** | **4** |

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia walioripotiwa mwezi wa Juni 2026 walikuwa 143 kati yao 61 walikuwa wapenzi sawa na asilimia 42.7, watu wasiojulikana walikuwa 36 sawa na asilimia 25.2, Jirani walikuwa 36 sawa na asilimia 25.2, watu wengine walikuwa saba (7) sawa na asilimia 4.9,  baba mzazi walikuwa wawili (2) sawa na asilimia 1.4 na mwalimu wa skuli alikuwa mmoja (1) sawa na asilimia 0.7

**Kielelezo 1.5: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia Juni, 2026**



## MAJALADA YA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOPOKELEWA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA ZANZIBAR JUNI, 2026

Jumla ya Majalada 57 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi wa Juni, 2026 ambayo yalihusisha makosa 64. Idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yametokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 41) sawa na asilimia 64.1 ya makosa yote ikilinganishwa na mikoa mwengine.

**Jadweli 2.1: Idadi ya Majalada na Mkosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa Juni, 2026**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Idadi ya Makosa |
|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 5 | 6 |
| Kusini Unguja | 4 | 4 |
| Mjini Magharibi | 35 | 41 |
| Kaskazini Pemba | 8 | 8 |
| Kusini Pemba | 4 | 4 |
| Makao Makuu | 1 | 1 |
| **Jumla** | **57** | **64** |

Kati ya Majalada 57 ya Udhalilishaji yaliyoripotiwa mwezi wa Juni, 2026, majalada 30 hayajatolea uamuzi, majalada 17 yameruhusiwa kwenda mahakamani, majalada nane (8) yamerudishwa Polisi kwa Upelelezi zaidi na majalada mawili (2) yamependekezwa kufungwa.

**Jadweli 2.2 Majalada ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa na Hatua, Juni 2026**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Yalioruhusiwa kwenda Mahakamani | Yaliopendekezwa kufungwa | Yaliorudi Polisi kwa Upelelezi | Hayajatolewa Uamuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 5 | 0 | 0 | 0 | 5 |
| Kusini Unguja | 4 | 2 | 0 | 0 | 2 |
| Mjini Magharibi | 35 | 7 | 0 | 6 | 22 |
| Kaskazini Pemba | 8 | 5 | 1 | 2 | 0 |
| Kusini Pemba | 4 | 3 | 1 | 0 | 0 |
| Mkao Makuu | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **57** | **17** | **2** | **8** | **30** |

Miongoni mwa makosa 64 ya udhalilishaji yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi Juni 2026, makosa mengi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 33) sawa na asilimia 51.6 ya makosa yote yaliyopokelewa.


**Jadweli 2.3: Idadi ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa, Juni 2026**

| Mkoa | Jumla ya makosa kwenye majalada yaliopokelewa | Kutorosha | Kumpa na kupokea ujauzito | Kubaka | Kulawiti | Shambulio la aibu/kukashifu | Kuingilia kinyume na maumbile | Kumuingilia mgonjwa wa akili |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 6 | 1 | 0 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini Unguja | 4 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini Magharibi | 41 | 3 | 0 | 18 | 7 | 5 | 8 | 0 |
| Kaskazini Pemba | 8 | 0 | 1 | 6 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kusini Pemba | 4 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Makao Makuu | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **64** | **6** | **1** | **33** | **9** | **5** | **9** | **1** |

## MASHAURI NA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOFUNGULIWA KATIKA MAHKAMA ZA UDHALILISHAJI ZANZIBAR KWA MWEZI WA JUNI 2026

Jumla ya mashauri 16 yamefunguliwa katika mahakama za udhalilishaji kwa mwezi wa Juni, 2026, ambapo yamehusisha makosa 19 . Mkoa wa Kusini Pemba umeripotiwa kuwa na mashauri mengi yaliyofunguliwa ambayo ni mashauri sita (6) yaliyohusisha makosa nane (8) ya udhalilishaji wa kijinsia sawa na asilimia 37.5 ya mashauri yote ikilinganishwa na mikoa mengine.

**Kielelezo 3.1: Mashauri ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyofunguliwa kwa Mkoa Juni, 2026**




Kati ya mashauri 16 yaliyofunguliwa katika Mahkama za udhalilishaji Zanzibar, mashauri yote bado yanaendelea.

**Jadweli 3.1: Idadi ya Mashauri ya Ukatili na Udhalilishaji Zilizofunguliwa katika Mahkama na hatua zilizochukuliwa Juni 2026**

| Aina ya makosa | Zilizopokelewa | Zinazoendelea | Zilizotiwa hatiani | | | | | Zisizo na hatia | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kifungo | Faini | Fidia | Kifungo na fidia | Faini na fidia | Zilizoachiwa huru | Zilizondoshwa /Zilozfutwa |
| kubaka | 10 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| kubaka na kumuingilia kinyume na maumbile | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| k/kubaka na shambulio la aibu | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| kutorosha | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutorosha na shambulio la aibu | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **16** | **16** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |

Jumla ya makosa 19 yaliyopokelewa katika Mahakama za udhalilishaji wa kijinsia, makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 12) sawa na asilimia 63.2 ya makosa yote yaliyopokelewa.

**Jadweli 3.2: Idadi ya Makosa ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia yaliyopokelewa Kimkoa Juni, 2026**

| Mkoa | Kaskazini Unguja | Kusini Unguja | Mjini Magharibi | Kaskazini Pemba | Kusini Pemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| kubaka | 1 | 1 | 2 | 4 | 4 | 12 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 3 |
| kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| Shambulio la aibu | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| **Jumla** | **1** | **1** | **5** | **4** | **8** | **19** |

## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu 21. Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 143 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa polisi kwa mwezi wa Juni, 2026 ambapo waathirika walikuwa 143. Waathirika wengi walikuwa watoto (waathirika 122 sawa na asilimia 85.3), wakifuatiwa na wanawake 17 (asilimia 11.9) na wanaume waliripotiwa wanne (4) sawa na asilimia 2.8.

Idadi ya matukio ya udhalilishaji kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 11.7 kufikia matukio 143 kwa mwezi Juni, 2026 ikilinganishwa na matukio 128 yaliyoripotiwa mwezi wa Mei, 2026. Matukio yaliyoripotiwa kupungua kwa mwezi Juni, 2026 yalikuwa matukio ya kujaribu kubaka, kutupa watoto, kutorosha, lugha ya matusi na shambulio la mtoto. Wilaya ya Magharibi ‘B’ imeripotiwa kuwa na idadi kubwa(matukio 26) ya matukio kwa mwezi wa Juni, 2026 na Wilaya ya Magharibi ‘A’ ilikuwa na idadi kubwa ya matukio kwa mwezi wa Mei, 2026 (matukio 25).

Matukio 122 kati ya matukio 143 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 85.3 ya matukio yote yaliyoripotiwa, aidha matukio 13 yamepelekwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (asilimia 9.1), matukio manne (4) yamepewa hati ya mashtaka (asilimia 2.8), matukio mawili (2) yapo mahakamani (asilimia 1.4) na matukio mawili (2) yamefungwa na polisi (asilimia 1.4).

Jumla ya Majalada 57 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi wa Juni, 2026 ambayo yalihusisha makosa 64. Idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yametokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 41) sawa na asilimia 64.1 ya makosa yote ikilinganishwa na mikoa mwengine. Kati ya Majalada 57 ya Udhalilishaji yaliyoripotiwa mwezi wa Juni, 2026, majalada 30 hayajatolea uamuzi, majalada 17 yameruhusiwa kwenda mahakamani, majalada nane (8) yamerudishwa Polisi kwa Upelelezi zaidi na majalada mawili (2) yamependekezwa kufungwa

Jumla ya mashauri 16 yamefunguliwa katika mahakama za udhalilishaji kwa mwezi wa Juni, 2026, ambapo yamehusisha makosa 19 . Mkoa wa Kusini Pemba umeripotiwa kuwa na mashauri mengi yaliyofunguliwa ambayo ni mashauri sita (6) yaliyohusisha makosa nane (8) sawa na asilimia 37.5 ya mashauri yote ikilinganishwa na mikoa mengine. Kati ya mashauri 16 yaliyofunguliwa katika Mahkama za udhalilishaji Zanzibar, mashauri yote bado yanaendelea.

**Kiambatanisho**

**Jadweli 1.0: Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Juni, 2026**

| Sehemu Zilotokezea | Nyumbani kwa Muathirika | | Nyumbani kwa Mtuhumiwa | | Nyumba za wageni/rafiki | | Sehemu za Kazi | | Majumba mabovu | | Vichakani | | Sehemu nyengine | | jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** |
| Kubaka | 1 | | 49 | | 3 | | 1 | | 10 | | 11 | | 3 | | 78 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 4 | | 0 | | 0 | | 4 | | 3 | | 2 | | 13 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | | 8 | | 0 | | 0 | | 4 | | 1 | | 0 | | 13 | |
| Kutorosha | 0 | 0 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 |
| Lugha ya matusi | 3 | 3 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 4 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 6 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 13 | 2 |
| Kutelekeza mtoto | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kuingilia maharimu | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mauaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| **Jumla** | **10** | **4** | **73** | **5** | **4** | **0** | **1** | **0** | **16** | **4** | **13** | **4** | **5** | **4** | **122** | **21** |

**Jadweli 2.0: Idadi ya Waaathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya kwa Aina ya Matukio na Wilaya Juni, 2026**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kujaribu kubaka | Kulawiti/ Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Lugha ya matusi | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Kutelekeza Mtoto | | Kuingilia maharimu | | Mauaji | | Kumpa na Kupokea ujauzito | |
| | | W'ke | W'ke | W'me | W'ke | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me |
| Kaskazini 'A' | 13 | 9 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 18 | 10 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 23 | 12 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 1 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Magharibi 'A' | 24 | 9 | 0 | 2 | 3 | 3 | 0 | 2 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Magharibi 'B' | 26 | 13 | 0 | 4 | 6 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 8 | 5 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 12 | 8 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 8 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **143** | **78** | **0** | **13** | **13** | **9** | **0** | **5** | **4** | **13** | **2** | **1** | **0** | **1** | **0** | **0** | **2** | **2** | **0** |

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mei, 2026 na Juni, 2026**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Mwanamme | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Mei-2026 | Juni-2026 | Mei-2026 | Juni-2026 | Mei-2026 | Juni-2026 | Mei-2026 | Juni-2026 | Mei-2026 | Juni-2026 |
| Kubaka | 65 | 78 | 5 | 7 | 60 | 71 | | | | |
| Kujaribu kubaka | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | | | | |
| Kulawiti/Kunajisi | 9 | 13 | | | | | 9 | 11 | 0 | 2 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 10 | 13 | 0 | 0 | 10 | 13 | | | | |
| Kutorosha | 11 | 9 | 1 | 0 | 10 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Lugha ya matusi | 13 | 9 | 5 | 3 | 3 | 2 | 4 | 4 | 1 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 15 | 15 | 4 | 4 | 10 | 9 | 0 | 2 | 1 | 0 |
| Kutupa watoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mauaji | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Shambulio la mtoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia maharimu | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutelekeza watoto | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 1 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **128** | **143** | **17** | **17** | **96** | **105** | **13** | **17** | **2** | **4** |

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Juni, 2025 na Juni, 2026**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Mwanamme | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 | Juni-2025 | Juni-2026 |
| Kubaka | 56 | 78 | 5 | 7 | 51 | 71 | | | | |
| Kujaribu kubaka | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | | | | |
| Kulawiti/Kunajisi | 7 | 13 | | | | | 6 | 11 | 1 | 2 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 5 | 13 | 0 | 0 | 5 | 13 | | | | |
| Kutorosha | 10 | 9 | 0 | 0 | 10 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Lugha ya matusi | 0 | 9 | 0 | 3 | 0 | 2 | 0 | 4 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 14 | 15 | 4 | 4 | 10 | 9 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Usumbufu wa kingono | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mauaji | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 |
| Uzinifu | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia maharimu | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutelekeza watoto | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 2 | 2 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **97** | **143** | **12** | **17** | **77** | **105** | **6** | **17** | **2** | **4** |

Jadweli 5.0 : Idadi ya Waathirika Wanawake na Wanaume wa Udhalilishaji wa Kijinsia, kwa Umri na Aina ya Matukio; Juni 2026

| Umri | 18-24 | | 25-35 | | 36-45 | | 46-64 | | 65+ | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** |
| Kubaka | 7 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 7 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 2 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 2 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | |
| Lugha ya matusi | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 |
| Kuingilia maharimu | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mauaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| **Jumla** | **14** | **2** | **3** | **0** | **0** | **2** | **0** | **0** | **0** | **0** | **17** | **4** |

**Jadweli 6.0: Muda wa Matukio ya Udhalilishaji Yalipotokea kwa Jinsi;  Juni, 2026**

| Muda Uliyotokea Matukio | 12:01 - 03:00 Asubuhi | | 03:01 - 6:00 Mchana | | 6:01 - 9:00 Jioni | | 9:01 - 12:00 Jioni | | 12:01 - 3:00 usiku | | 3:01 - 09:00 Usiku | | 6:01 - 09:00 Usiku | | 09:01 - 12:00 Asubuhi | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** |
| Kubaka | 2 | | 6 | | 21 | | 14 | | 29 | | 6 | | 0 | | 0 | | 78 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 2 | | 0 | | 1 | | 2 | | 6 | | 2 | | 0 | | 0 | | 13 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | | 0 | | 2 | | 5 | | 5 | | 1 | | 0 | | 0 | | 13 | |
| Kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 |
| Lugha ya matusi | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 2 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 4 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 1 | 0 | 2 | 0 | 4 | 1 | 2 | 1 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 | 2 |
| Kutelekeza mtoto | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kuingilia  maharimu | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mauaji | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| **Jumla** | **3** | **3** | **9** | **0** | **31** | **5** | **26** | **5** | **44** | **6** | **9** | **2** | **0** | **0** | **0** | **0** | **122** | **21** |

**Jadweli 7: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Yaliyoripotiwa Polisi kwa Miezi , 2020-2026**

| Miezi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 116 | 122 | 65 | 173 | 171 | 103 | 113 |
| Februari | 155 | 100 | 100 | 164 | 175 | 107 | 98 |
| Machi | 136 | 141 | 82 | 155 | 125 | 78 | 103 |
| Aprili | 95 | 108 | 68 | 148 | 148 | 102 | 129 |
| Mei | 118 | 66 | 74 | 154 | 172 | 107 | 128 |
| Juni | 102 | 97 | 97 | 127 | 174 | 97 | 143 |
| Julai | 114 | 108 | 78 | 168 | 165 | 107 | |
| Agosti | 116 | 96 | 131 | 175 | 157 | 116 | |
| Septemba | 115 | 90 | 170 | 157 | 148 | 106 | |
| Oktoba | 103 | 107 | 164 | 199 | 147 | 99 | |
| Novemba | 92 | 90 | 177 | 172 | 136 | 107 | |
| Disemba | 101 | 97 | 154 | 162 | 91 | 99 | |
| **Jumla** | **1,363** | **1,222** | **1,360** | **1,954** | **1,809** | **1,228** | **714** |

**Jadweli 8: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Yaliyoripotiwa Polisi kwa Miezi na Wilaya, 2026**

| Miezi | Kaskazini 'A' | Kaskazini 'B' | Kati | Kusini | Mjini | Magharibi 'A' | Magharibi 'B' | Wete | Micheweni | Chake Chake | Mkoani | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 5 | 7 | 9 | 2 | 18 | 23 | 18 | 11 | 9 | 6 | 5 | 113 |
| Februari | 3 | 5 | 10 | 2 | 18 | 21 | 17 | 7 | 6 | 7 | 2 | 98 |
| Machi | 8 | 9 | 10 | 1 | 17 | 19 | 18 | 11 | 2 | 6 | 2 | 103 |
| Aprili | 8 | 7 | 10 | 3 | 25 | 23 | 21 | 9 | 3 | 10 | 10 | 129 |
| Mei | 6 | 8 | 13 | 2 | 20 | 25 | 24 | 12 | 4 | 6 | 8 | 128 |
| Juni | 13 | 4 | 18 | 3 | 23 | 24 | 26 | 8 | 4 | 12 | 8 | 143 |
| Julai | | | | | | | | | | | | |
| Agosti | | | | | | | | | | | | |
| Septemba | | | | | | | | | | | | |
| Oktoba | | | | | | | | | | | | |
| Novemba | | | | | | | | | | | | |
| Disemba | | | | | | | | | | | | |
| **Jumla** | **43** | **40** | **70** | **13** | **121** | **135** | **124** | **58** | **28** | **47** | **35** | **714** |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendochochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi auya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wangono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile nashambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hiiya mwaka 2004. Sheria hii imetungwapamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenyeshehemu ya kumi na tatu (Section thirteen)ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendovya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyohaviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishajiwa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wakijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadikifungo cha maisha.

**Kwa Ufafanuzi zaidi Tafadhali Wasiliana na:-**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua,2321,
Simu: +255242231869
Barua pepe: cgs@ocgs.go.tzWebsite:
http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.comNukushi:
024223136
**MMP, Zanzibar.**